

Makazi ya Wanajeshi Wastaafu ya Rhode Island



Makazi ya Wanajeshi Wastaafu ya Rhode Island (RIVH)

hutoa utunzaji wa uuguzi na huduma za wakaazi kwa wanajeshi wastaafu waliohusika katika vita wanaostahiki. Huduma za kijamii, matibabu, uuguzi na urekebishaji zinapatikana ili kuboresha hali njema ya mwanajeshi mstaafu ya kimwili, kihisia na kiuchumi. Huduma ni pamoja na utunzaji wa kimatibabu, tiba ya kimwili, huduma ya afya ya akili, meno, eksirei, na huduma za duka la dawa. Ufikiaji wa shughuli ndani na nje ya eneo hilo, kinyozi, duka la zawadi, benki, na usafiri wa kwenda na kutoka Kituo cha Matibabu cha Providence VA na kliniki zake zinazoshirikiwa katika Providence pia zinapatikana.

Wanajeshi wastaafu wanaostahiki hulipa tathmini kulingana na asilimia ya mapato yao kwa ajili ya makazi na utunzaji wao. RIVH si kituo cha Medicaid. Hakuna haja ya kutumia rasilimali za kifedha hadi mwisho ili kuhitimu. RIVH hupokea ufadhili wa ziada kutoka kwa jimbo na Idara ya Masuala ya Wanajeshi Wastaafu wa Marekani.

Nani anastahiki?

- Wanajeshi wastaafu walioruhusiwa kuwacha kazi kwa heshima zote za kijeshi ambao walihudumu kazi wakati wa vita, na
- Waliojiunga na jeshi wakati wakiwa wakazi wa Rhode Island au waliishi Rhode Island kwa angalau miaka miwili kabla ya tarehe ya kutuma maombi kwa RIVH.

Kwa habari zaidi, piga simu 401-253-8000.

Huduma inayohusiana

Idara ya Masuala ya Wanajeshi Wastaafu ya Marekani inafanya kandarasi na hospitali za kutunza wazee za jamii ili kutunza wanajeshi wastaafu.

Jinsi ya kupata huduma hizi

Wanajeshi wastaafu wanaovutiwa au wanafamilia wa wanajeshi wastaafu wanaweza kuwasiliana na RIVH kwa ombi na/au kuratibu ziara kwa kupiga simu 401-253-8000.